



# ARUSHA MEAT COMPANY LTD

P. O. BOX 14167

ARUSHA

TANZANIA

E-mail: [arushameatcompany@yahoo.com](mailto:arushameatcompany@yahoo.com)

TEL: +255 272970304

Mob: +255734026767

**KUMB. NA. AMCO/STF/O10/39**

**DATE: 06/02/2023.**

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.**

Arusha Meat Company Limited ni Kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za Makampuni ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inajishughulisha na huduma ya uchinjaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo. Aidha Kampuni hii pia huchakata nyama kwa ajili ya kutengeneza bidhaa mbalimbali. Arusha Meat Co. Ltd inakaribisha waombaji wenye sifa kujaza nafasi mbili (2) zilizo wazi kama ifuatavyo:

### **1.1. MHASIBU (ACCOUNTANT) NAFASI MOJA (1).**

### **1.2. MAJUKUMU YAKE YATAKUWA KAMA IFUATAVYO:**

- i. Kuidhinisha hati za malipo.
- ii. Kuandaa taarifa ya mapato na matumizi ya mwezi.
- iii. Kusimamia wahasibu wasaidizi katika kazi zao za kila siku.
- iv. Kuandaa taarifa ya maduhuli.
- v. Kushirikiana na Mkuu wa Idara ya Fedha kuhakikisha shughuli za uendeshaji wa Kampuni zinafuata kanuni zote za fedha.
- vi. Kufanya shughuli zote zinazohusiana na malipo ya kodi kwa TRA na kuandaa nyaraka kwa ajili ya Ukaguzi wa hesabu.
- vii. Kusaidia usimamizi katika mchakato wa kufanya maamuzi wakati wa uandaaji wa bajeti na makisio ya mapato ya Kampuni kwa mwaka husika.
- viii. Kufuata sheria na kanuni zote za uendeshaji wa biashara, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha leseni na vibali vyote vinalipiwa kwa wakati kulingana na miongozo ya Kampuni.

- ix. Kukusanya, kuchambua, na kutoa taarifa za fedha mara kwa mara, kama vile taarifa za faida na hasara pamoja na kufunga mahesabu.
- x. Utafanya jukumu lingine kama utakavyopangiwa na Mwajiri.

### **1.3. SIFA ZA MWOMBAJI.**

- i) Awe na shahada au (Advanced-Diploma) katika fani ya Uhasibu.
- ii) Mwenye cheti cha taaluma ya uhasibu CPA (T) au sifa inayolingana nayo kwa kutambuliwa na NBAA atapewa kipaumbele.
- iii) Awe na uzoefu usiopungua miaka miwili (2) wa kufanya kazi katika fani ya uhasibu.
- iv) Awe na umri usiozidi miaka 45.

### **1.4. MSHAHARA:**

Kwa kuzingatia ngazi za Mishahara ya Arusha Meat Co. Ltd yaani ngazi **AMC 7.**

### **2.1. MTUNZA STOO (STORE-KEEPER) NAFASI MOJA (1).**

### **2.2. MAJUKUMU YATAKUWA KAMA IFUATAVYO:**

- i. Kuandaa na kutunza kumbukumbu zote za vifaa/bidhaa zinazolingana orodha /mtiririko (stock movement).
- ii. Kutoa vifaa kutoka stoo kwenda kwa watumiaji kwa kuzingatia utaratibu ulioidhinishwa.
- iii. Kupokea na kukagua ubora wa bidhaa/vifaa vinavyoingia kwa ajili ya matumizi mbali-mbali ya Kampuni.
- iv. Kupitia mara kwa mara mahitaji ya malighafi/vifaa kulingana na mahitaji na kutoa taarifa kwa Mkuu wa idara husika ili kuhakikisha uwepo wa mali ghafi/vifaa vya kutosha.
- v. Kuandaa na kutunza taarifa za manunuzi ya vifaa na malighafi ya manunuzi mbali-mbali.
- vi. Kuandaa na kutunza kumbukumbu za vifaa/malighafi zilizopokelewa stoo.

### 2.3. SIFA ZA MWOMBAJI.

- a) Awe na astashahada katika Manunuzi na Ugavi kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali au Bodi ya wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) "Foundation stage I and II".
- b) Mwenye uzoefu usiopungua mwaka mmoja (1) katika fani hiyo atapewa kipaumbele.
- c) Awe na ujuzi wa kutumia Kompyuta.
- d) Awe na umri usiozidi miaka 45.

### 2.4. MSHAHARA:

Kwa kuzingatia ngazi ya Mishahara ya Arusha Meat Co. Ltd yaani ngazi ya **AMC 2**.

### MASHARTI YA JUMLA KWA NAFASI ZILIZOTANGAZWA.

- i. Waombaji wawe raia wa Tanzania.
- ii. Waombaji waambatanishe Cheti cha kuzaliwa.
- iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu pamoja na barua iliyoandikwa kwa mkono na kusainiwa.
- iv. Anuani na namba ya simu ya mwombaji na picha moja "Passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
- v. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, nakala za vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika vyeti vya kitaaluma (professional certificate) kutoka bodi husika na viwe "Certified".
- vi. "Testimonials" "provisional results" "statement of result" hati matokeo za kidato cha nne na sita **HAVITAKUBALIWA.**
- vii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU, NECTA, NACTE).
- viii. Mwombaji atajigharamia mwenyewe wakati wa usaili.
- ix. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATAPOKELEWA.**
- x. Ajira hii ni ya mkataba wa muda maalum.

**NB:** Barua zote za maombi zitumwe kwa njia ya Posta kwa anuani ifuatayo:

MENEJA MKUU,  
ARUSHA MEAT CO. LTD,  
S.L.P 14167,

**ARUSHA-TANZANIA.**

**NB:** Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **19/02/2023.**

Imetolewa na: -

  
STEPHEN L. SULTAN  
**MENEJA MKUU**  
ARUSHA MEAT CO. LTD



**Nakala:**

- Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi (AMCL),  
S.L.P 14167,  
**ARUSHA.**
- Mbao za matangazo.
- Tovuti ya Kampuni.